

Haki za Binadamu British Columbia: Ubaguzi kwa sababu ya utambulisho au kujieleza kijinsia

Karatasi hi ya ukweli imetengenezwa ili kukusaidia kuelewa ubaguzi kwa sababu ya utambulisho au kujieleza kijinsia katika BC. Ikiwa una maswali yoyote kuhusu hali yako, tafadhali wasiliana na **BC Human Rights Clinic (Kilinki ya BC ya Haki Za binadamu)**. Maelezo zaidi kuhusu mawasiliano yanapatikana mwishoni mwa karatasi hii ya ukweli.

British Columbia ina sheria ya kulinda na kukuza haki za binadamu. Hii inaitwa *BC Human Rights Code au Code (kanuni)*. Kanuni inakulinda dhidi ya kutendewa mabaya au kutendewa tofauti kwa sababu ya utambulisho wako au unavyojieleza kijinsia. Inakuruhusu kuripoti lalamiko kwenye BC Human Rights Tribunal (mahakama ya haki za binadamu katika BC) ikiwa unaamini kwamba umebaguliwa.

Code (kanuni) hii pia inakulinda dhidi ya **kulipizwa kisasi** ikiwa umeripoti, au unafikiria kuripoti, lalamiko au umehusika kwa njia yoyote ile. **Kulipiza kisasi** ni kama kuna mtu anajaribu kukudhuru au kujaribu kukufuatilia kwa nia ya kukudhuru au kukulipiza.

Ufafanuzi uliotumika katika karatasi hii ya ukweli

Utambulisho wa jinsia ni hisia za mtu binafsi kama mwanamke, mwanamme au wote viwili, katikati au siyo kati yao. Inajumuisha watu ambao wanajihisi kuwa **si wanaume au wanawake (transgender)**. Utambulisho wa jinsia inaweza kuwa sawa au tofauti na jinsia wakati wa kuzaliwa.

Kujieleza kijinsia ni namna ambavyo mtu anajiwasilisha kijinsia. Hii inajumuisha tabia na mwonekano, pamoja na nguo, nywele, urembo, lugha ya mwili na sauti. Hii inaweza vile vile kujumuisha jina lake na kijina (he, she, they). Namna ambayo mtu anavyowakilisha jinsia yake siyo lazima ioanishwe na utambulisho wa jinsia yake.

Kwa mfano, kama utambulisho wa jinsia wa mtu ni mwanamme, kujieleza kwa jinsia ni wa kiume pale ambapo kawaida anonyesha sifa katika tabia, mavazi, na/au utaratibu. Utambulisho wa jinsia ni tofauti na mwelekeo wa kijinsia.

Trans au Transgender ni msamiati mpana unaoeleza watu wenye utambulisho wa jinsia tofauti na kujieleza kijinsia ambayo hailingani na mawazo ya jumla kuhusu maana ya msichana/mwanamke au mvulana/mwanamme. Kwa mfano watu wanojitambulisha kama wabadili jinsia (transgender), wabadili mke (transwoman, mme kuelelekea mke), wabadili mme (trans man, mke kuelelekea mme), wabadili jinsia (transsexual), wavuka-mavazi (cross-dresser), wasiozingatia jinsia (gender no-conforming), jinsia tofauti (gender variant) au jinsia zisizo za kawaida (gender queer). Kuwa transgender haina maana ya mwelekeo wa jinsia.

Ni nini ubaguzi wa utambulisho au kujieleza kijinsia

Kila mtu anayo haki ya kufafanua utambulisho wa jinsia yao na kujieleza kijinsia. Watu wanojibadilisha lazima watambuliwe na kutendewa kulingana na jinsia wanazoishi na wanazopendelea kujieleza.

Ubaguzi unatokea pale mtu anapotendewa vibaya au ananyimwa huduma au mafao kwa sababu ya utambulisho au kujieleza kijinsia.

Ubaguzi kwa sababu ya utambulisho au kujieleza kijinsia unaweza kutokea katika njia nyingi, zikiwemo:

- Unaitwa majina ya kuchukiza.
- Unawekwa katika utani, sura, barua pepe, mitandao isiyofaa.
- Unanyimwa huduma kwa sababu ya utambulisho au kujieleza kijinsia.

- Unafukuzwa kazi au kutoajiriwa au kupandishwa cheo kwa sababu ya utambulisho au kujieleza kijinsia.
- Unakataliwa pango la nyumba kwa sababu ya utambulisho au kujieleza kijinsia.

Nitajuaje kama nina malalamiko ya Haki za Binadamu?

Kuripoti malalamiko kwenye *BC Human Rights Code (Kanuni ya haki za binadamu BC)*, yote yafuatayo lazima yawe ya kweli:

- ✓ Umetendewa ubaya au umenyimwa mafao.
- ✓ Kuna uhusiano baina ya namna ulivyotendewa (vibaya au kunyimwa mafao) na utambulisho au kujieleza kijinsia kwako.
- ✓ Vitendo hivyo viwe vimetokea katika sehemu kama vile kazini, dukani au mgahawani, au baina ya mwenye nyumba na mpangaji.

Lazima uripoti malalamiko yako katika muda wa miezi sita ya tukio kutokea. (Kumbuka: kuna baadhi ya kesi za kipekee zisizo fuata muda huo uliyowekwa.) Kuripoti lalamiko kuanzisha mchakato wa kisheria sawa na hatua za hakama. Mtu mwenye kuripoti malalamiko anaitwa **mlalamikaji**. Kwa maelezo ya ujumla kuhusu Human Rights katika BC (Haki za Binadamu BC), tafadhali tazama karatasi ya ukweli kuhusu **Haki za binadamu British Columbia: Nini unahitaji kujua**.

Wapi naweza kupata usaidizi?

Unaweza kupata habari kupitia **Kliniki ya Haki za Binadamu ya BC**. Watu wa Kliniki wanaweza kukusaidia kuelewa *Kanuni* za Haki za binadamu au kushughulikia lalamiko la haki za binadamu kijimbo. Unaweza ukafuzu kupata huduma zingine vile vile. Zungumza na watu wa Kliniki kuona kama unastahili.

Kliniki ya Haki za Binadamu BC

300-1140 West Pender Street
Vancouver, BC V6E 4G1
Tel: 604 622-1100
Fax: 604 685-7611
Toll Free: 1-855-685-6222
Web: www.BCHRC.net

Ikiwa kuna mtu ameripoti malalamiko juu yako, basi wewe ni **mhojiwa**. **Wahojiwa** wote kwenye jimbo na eneo la Victoria wanaweza kupata maelezo zaidi kwa kuwasiliana na:

University of Victoria

Law Centre Clinical Law Program
Suite 225 – 850 Burdett Avenue
Victoria, BC V8W 1B4
Phone: 250 385-1221
Toll Free: 1-866-385-1221
E-mail: reception@thelawcentre.ca

Unaweza kuelekezwa kwa **BC Human Rights Tribunal (Mahakama ya BC ya Haki za Binadamu)** kuwasilisha malalamiko yako.

BC Human Rights Tribunal

Suite 1170 – 605 Robson Street
Vancouver, BC V6B 5J3
Phone: 604 775-2000
Toll Free (in BC): 1- 888- 440-8844
TTY (walio kuwa na matatizo ya kusikia):
604 775-2021
Web: www.bchrt.gov.bc.ca